

# Kudumisha Lugha ya Familia Yako

Kudumisha lugha ya familia yako kunajenga msingi wa maendeleo yote ya baadaye ya lugha. Mtoto wako anaweza kujifunza lugha nyingi kwa urahisi anapopata fursa za kuona, kusikia na kuwasiliana na miundo thabiti ya lugha.

Wataalam wa watoto wadogo katika Jiji la Victoria wanaongozwa na *Mfumo wa Kujifunza na Maendeleo ya Watoto Wadogo Victoria* (Victorian Early Years Learning and Development Framework) (VEYLDF). Mfumo huu unatambua lugha nyingi kama nyenzo muhimu na unaweka matarajio kwamba watoto watasaidiwa kudumisha lugha ya familia, kujifunza Kiingereza kama lugha ya ziada, na kujifunza lugha nyingine isipokuwa Kiingereza wanapohudhuria programu za Elimu na Malezi ya Watoto Wadogo (VEYLDF, 2016).

Kuna faida nyingi kwa mtoto wako anapodumisha na kuendelea kukuza lugha ya familia yake:

- Mtoto wako anaweza kupanua uwezo wake wa kubadilika na kukua kimawazo kujitia matumizi ya lugha ya familia yako.
- Kudumisha lugha ya familia yako ni muhimu kwa uhusiano wa familia, kujenga mahusiano na kuhisi kuwa wewe ni sehemu yake.
- Lugha ya familia ina uhusiano usioweza kutenganishwa ambao unahusiana na utambulisho, utamaduni na ustawi wa mtoto wako.
- Ufasaha katika lugha ya familia yako humsaidia mtoto wako kujifunza lugha za ziada kama vile Kiingereza.

VEYLDF (2016) inawaeleza waelimishaji kwamba ‘ujifunzaji na udumishaji wa lugha za kwanza au za nyumbani una jukumu muhimu na endelevu katika kujenga utambuzi’ (pg. 18). Hata hivyo, kipengele muhimu cha kusaidia ukuzaji wa Kiingereza kama lugha ya ziada ni kwa waelimishaji na familia kushiriki katika ushirikiano ili kuhimiza na kuwasaidia watoto kudumisha na kuendeleza lugha ya familia yao.

## Kukuza Kiingereza kama Lugha ya Ziada katika Elimu ya Awali na Mazingira ya Malezi

Mtoto wako atakuwa na fursa nyingi za kujifunza Kiingereza katika mazingira ya Elimu ya Awali na Malezi katika Jiji la Victoria. Utafiti unatuambia kwamba ‘watoto

wanaweza kujifunza Kiingereza (au lugha nyingine) kwa mafanikio kama lugha ya ziada kujitia kuwa karibu na lugha husika, uundaji wa lugha dhahiri na ufundishaji wa lugha, na muda unaofaa wa kujifunza lugha mpya’ (VEYLDF, 2016, pg. 22).

Kujua lugha moja kunaweza kuwasaidia watoto kuelewa jinsi lugha nyingine zinavyofanya kazi. Ujuzi ambao watoto wanakuza katika lugha moja unaweza kuhamishiwa kwenye lugha mpya. Kujitia lugha ya familia ambapo watoto wanaweza kuelewa lugha mpya, kanuni zake na msamati. Mtoto wako anapokuwa amezama katika mazingira ya lugha ya Kiingereza, atapata fursa ya kusikia Kiingereza katika miktadha mingi tofauti. Watataka kujunga na kucheza na watoto wengine na waelimishaji watatoa mifano mizuri na fursa nyingi kwa mtoto wako kusikia na kufanya mazoezi ya Kiingereza.

Maarifa ya lugha hukua kwa kasi inayolingana na tajriba ya lugha ya awali ya mtoto, kuwa karibu na lugha mpya na mazingira mapya anamosomea. Watoto wanaojifunza lugha nyingi kwa wakati mmoja wanaweza, kwa muda fulani, kuzungumza zaidi lugha moja kuliko nyingine. Mwanzo watoto wanaweza kuchanganya lugha wanapozungumza. Wanaweza kujua neno kwenye lugha moja na wasijue kwenye lugha nyingine. Ili kudumisha ufasaha wa mazungumzo yao, hutumia maneno wanayoyajua. Huu ni ujuzi wa asili na unaonyumbulika ambao unakua kwa watoto kadri wanapotumia lugha zao katika miktadha ya lugha nyingi.

## Kumbuka...

Inachukua muda kukuza ufasaha wa mazungumzo katika lugha mpya na watoto wanahitaji muda na usaidizi usio na shinikizo kutoka kwa watu wazima wanaowazunguka wanapopitia michakato ya kujifunza lugha ya ziada.

Ni Haki ya watoto kutumia na kujifunza lugha ya familia (UNCRC, 1989).

### Marejeo

Department of Education and Training, 2016. *Victorian Early Years Learning and Development Framework*.

UNICEF, 1989. *United Nations Convention on the Rights of the Child* (UNCRN).